BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TATHMINI YA WATAHINI KUHUSU UFAULU WA WATAHINIWA WA KIDATO CHA NNE, 2014

## 021 KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TATHMINI YA WATAHINI KUHUSU UFAULU WA WATAHINIWA WA KIDATO CHA NNE, 2014

# 021 KISWAHILI

## (Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2015

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO


DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 1

2.1 Sehemu A: Ufahamu ........ 1

2.1.1 Swali la 1: Ufahamu na Ufupisho ........ 1

2.1.2 Swali la 2: Ufupisho ........ 4

2.2 Sehemu B: Sarufi na Utumizi wa Lugha ........ 8

2.2.1 Swali la 3: Utata katika Mawasiliano. ........ 8

2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno ........ 10

2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno ........ 11

2.2.4 Swali la 6: Uundaji wa Maneno ........ 14

2.2.5 Swali la 7: Aina za Maneno ........ 15

2.3 Sehemu C: Uandishi ........ 16

2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Insha ........ 16

2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Hotuba ........ 20

2.4 Sehemu D: Maendeleo Ya Kiswahili ........ 23

2.4.1 Swali la 10: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili. ........ 23

2.5 Sehemu E: Fasihi Kwa Ujumla ........ 27

2.5.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi ........ 27

2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi ........ 30

2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya ........ 38

2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 44

2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Kazi za Kifasihi ........ 49

3.0 HITIMISHO ........ 55

4.0 MAPENDEKEZO ........ 56

Kiambatisho ........ 57

# DIBAJI


Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Nne kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu katika mtihani wa somo hilo kwa wanafunzi, walimu, wazazi waandaaji wa sera na jamii kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa yale ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika elimu ya Sekondari.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vibaya au vizuri katika mtihani wao. Taarifa inaonesha baadhi ya sababu zinazofanya watahiniwa wengi kupata alama za juu katika majibu yao. Sababu hizo ni kama vile kuelewa matakwa ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha na kuwa na uelewa wa dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili. Aidha, taarifa hii inaonesha sababu zinazofanya watahiniwa wachache kutokufanya vizuri kwenye baadhi ya maswali. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayooendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania litapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na umma kwa ujumla ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za watahini zitakazofuata.

Mwisho Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, walimu wa somo na wengine wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii. Tunapenda vilevile kutoa shukrani zetu za pekee kwa wafanyakazi wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika taarifa hii.



Dr. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa watahiniwa wa mtihani wa Kidato cha Nne wa mwaka 2014 kwa somo la Kiswahili. Mtihani huo ulikuwa na maswali 15 yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Sarufi na Utumizi wa Lugha*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili* pamoja na *Fasihi kwa Ujumla*. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A, B na D, swali moja (1) kutoka sehemu C na maswali matatu (3) kutoka sehemu E. Swali la 15 lilikuwa la lazima.

Mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2014 ulifanywa na watahiniwa 240,334. Kati ya watahiniwa hao, waliofaulu ni 167,365 sawa na asilimia 69.66 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, yaani waliopata daraja A hadi D na waliopata daraja E na F ni asilimia 30.34. Kiwango hicho cha ujumla cha ufaulu kilikuwa ni cha juu ukilinganisha na kilivyokuwa mwaka 2013. Aidha, asilimia ya waliofaulu kwa mwaka 2014 ilikuwa 69.66 ambayo ni ya juu kuliko asilimia ya waliofaulu mwaka 2013 ambapo asilimia ya ufaulu ilikuwa 51.05.

Taarifa hii inaelezea uchambuzi wa maswali ya mtihani na majibu yaliyotolewa na watahiniwa. Sampuli za majibu ya watahiniwa pia zimewekwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kile kilichofanywa na watahiniwa. Uchambuzi huu unatarajiwa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi walioko shuleni na kutoa matokeo makubwa kwa siku za usoni.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Ufahamu

#### 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu na Ufupisho

Swali hili lilihusu mada ya *Ufahamu na Ufupisho* na lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Swali hili lilikuwa na vipengele (a) hadi (d) na lilikuwa na jumla ya alama 05.


Vipengele (a) hadi (c) vilipima maarifa na kipengele (d) kilipima tathmini.

Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kueleza maana za maneno aliyopewa kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Maneno hayo ni (*i) fadhaa, (ii) madhila, (iii) kuadhiriwa, (iv) ima faima (v) kigeugeu na (iv) kigegezi.* Kipengele (a) kilikuwa na jumla ya alama 03, kila maana ya neno ikiwa imebeba alama 00½. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kueleza mchanganyiko wa fikra walizonazo wana wa Kusadikika kuhusu Karama, nacho kilikuwa na alama 00½. Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kutoa sababu mbili zinazoelezea ni kwanini bidii ya mjumbe wa kusini ililinganishwa na bidii ya siafu. Kila sababu ilikuwa na alama 00½ hivyo vyote viwili vilikuwa na alama 01. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kueleza ujumbe wa mwandishi na kilikuwa na alama 00½.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 89.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, ambapo kati yao asilimia 50.3 walipata alama 0 hadi 01, miongoni mwao asilimia 9.2 walipata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kujibu vipengele vyote kwa usahihi. Baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kueleza maana za maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Watahiniwa wengine walijibu baadhi ya vipengele vya swali na kuviacha vingine bila kujibu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika maana zisizo sahihi kwa kipengele (a) na alishindwa kabisa kujibu vipengele (b) hadi (d) hivyo alipata alama 0.

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kipengele (a) pekee na kuacha vipengele (b) hadi (d) hata hivyo majibu aliyotoa kwa kipengele (a) hayakuwa sahihi.


**Kielelezo 1.1**


1. (i) i/ Fadhaa
Ni hali ya kuwa na Iman
(ii) Madhila
Ni kuwa na mambo
(iii) Kuadhiriwa
Ni ile hali ya kuumiswa
iv/ Ima faima
Ni hali ya kuendelea
V/ Kigeugeu
Ni hali ya kiherehere
Vi/ kigegeri
Ni hali ya kutokujisikia Vibaya

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kwa kipengele (a). Hata hivyo, licha ya majibu kutokuwa sahihi, yalikuwa na dosari katika uandishi. Kwa mfano kipengele (i) mtahiniwa ameandika neno '*iman*' akikusudia kuandika '*imani*' na (iii) neno '*kuumiswa*' badala ya '*kuumizwa*.' Aidha, mtahiniwa huyo hakujibu kabisa kipengele (b) hadi (d).

Watahiniwa 49.7% ndio walioweza kujibu vizuri maswali ya kipengele (a) hadi (d). Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 43.5 walipata alama $01^{1}/_{2}$ hadi $02^{1}/_{2}$, kwa kuwa walitoa majibu sahihi kwa vipengele vichache vya swali. Asilimia 6.2 walipata alama kati ya 03 hadi $04^{1}/_{2}$, kwa sababu waliweza kutoa maana sahihi za maneno ya kipengele (a) na kwa vipengele (b) hadi (d) pia walitoa majibu sahihi. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi katika vipengele vingi lakini alishindwa kutoa maana sahihi ya kipengele (a) (vi) tu.

**Kielelezo 1.2**


1. (a) (i) Fadhaa ni hali ya kuumia moyoni juu ya jambo fulani
(ii) Machila ni majanga
(iii) Kuadhiriwa ni kuaibika mbele za watu
(iv) Ima fa ima ni harakaharaka
(v) Kigeugeu ni kubadili kitu bila ya kuichia toka moyoni
(vi) Kigegezi ni kutojali

(b) Kuna wengine ambao walikuwa wanamuona Karama kama ni mtu bora na anayeweza kuokoka lakini kuna wengine walimwona kama mjinga aliye anayeachoza na hatari iliyo mbele yake

(c)(i) Alikuwa anaficha hatari iliyowakuta wenzake lakini baada alijitolea kwa moyo mweupe na mkunjufu kuingia kwenye kazi ileile iliyofanywa na wenzake.
(ii) Alionyesha ujasiri na kutoogopa chochote katika kutetea maslahi ya wenzake

(d) Ujumbe wa mwandishi wa kifungu hiki unahusu kujitoa muhanga na kuwa mzalendo wa kutetea hali yako na ya wenzako.

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali vizuri.

### 2.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali hili lilihusu mada ya *Ufahamu na Ufupisho* na lililenga kupima ujuzi wa matumizi ya taratibu za ufupisho. Swali lilikuwa na alama 05 na lilimtaka mtahiniwa kufupisha habari aliyoisoma kwa maneno yasiyopungua 150 na yasiyozidi 200. Swali hili lilijibiwa na asilimia 61.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani.

Asilimia 41.8 ya watahiniwa walijibu vibaya swali hili na walipata alama 0 hadi 01, kwa kuwa hawakuzingatia kanuni za ufupisho ambazo ni: *kutumia maneno yao bila kupotosha kiini cha habari ya awali, kuzingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki, kuzingatia taratibu za uandishi na matumizi*

*sahihi ya lugha na idadi ya maneno*. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakufuata taratibu za ufupisho, aidha ufupisho wake una maneno zaidi ya 200.

**Kielelezo 2.1**

2 Karibu masikio ya watu wa mahali
pengi yalijaa habari za karama na msiba
wa ndoe. Umaarufu wake wa ghafla ulio
ngurumwa karibu na mbali. Mtu yeyote w
a destura anapozuka katika umaarufu
huyavuta masikio na macho ya watu
wengi kwa sababu jambo kama hili
hutokea nadra sana kwa watu ambao b
ahati mbaya imeshughulika kuwaweka
nyuma. ~~kwa ta~~ kwa hiyo siku ya fat
ya baruna alitunukiwa na Mfalme w
atu wenye vyeo mbalimbali pamoja na
nusu moja ya umati, Msubwa wa kusadi k
ika fikra zilizochangika zilizashika uma
ti huu

Walioikuwa wakimtarajamia kuokoka
walikuwa na wasiwasi wao na wale walioku
wa wakimtarajamia kuanguka walikuwa na
fadhaa yao walakini hapana mtu hata mmoja
aliyepata kulisema wazo lake

Bila ya kujua aliyojaliwa Karama
aliendelea kusema moyo ya barua, "watu
wanateswa ndio, wanaoyajua mateso yao".
Kusadikika ilikuwa chimi ya mateso wa
kuwa sana maisha yao yalianyukwa na
maradhi na mauti daima usio kwisha ndi
aliyo karibu kugeuka janga na mvumbi
na madhila mengine mateso yaliyowakabili
watu.

Kusadikika ilikosi kuona mjumbe

2. baadhi ya nyumba kuadhiriwa na ku
adhibiwa vibaya. Kama washauri hawa
kudhuriwa na hili lakini watu wengine
walidhuriwa sana.
Hili lilipotokea serikali iliombwa
imafanya kufanya nyumba nyingine.
Basi nyumba ya tatu ilitafutikana ajito
lee mwenyewe kwa nyumba na kusini. W
ito ~~na~~ wa nyumba ya tatu ulitikiwa na
kabuli; Mtu mwenye busara naye na m
chezi yule alipatikana upesi kabisa ku
kiko kilivyokuwa kwa mara ya pili na ya
kwanzwa
Hapana fisho liwezako kuukomesha
mwendo huu. Kwa hakika utahukulira
kuwako duniani mpaka macho yaukome
kabisa, na labda watatu huo duniani hili
limekuwa njema kama kumani wengo ku
wo. Burhani na fadhili walitoa sada
ka zao bora ili kuyanimiza majilio ya
wakati ulioteketikama sana
Kama yulikanavyo, kusini ni upa
nde wa dunia yukokanao matufani m
akukuwa na bandi kali sana kabuli ali
yakabili mashaka haya bila ya kige
ugeu. Maam alikuwa kuwa Mtu aliye
kuwa akinywa uchungu bila ya ki
gegezi. Mara mbili alikamatwa na ka
funywa mahabusu

Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye badala ya kufupisha alinakili maneno kama yalivyokuwa kwenye habari ya awali.

Asilimia 58.2 ya watahiniwa waliweza kuandika ufupisho kwa kuzingatia taratibu za uandishi. Miongoni mwao asilimia 48.6 walizingatia baadhi tu ya taratibu na kukiuka zingine hivyo walipata alama $01^1/_2$ hadi $02^1/_2$. Asilimia 9.6 tu ndio

waliozingatia kwa kiasi kikubwa taratibu za uandishi hivyo kupata alama 03 hadi $04^{1}/_{2}$. Kielelezo 2.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyezingatia taratibu za uandishi wa ufupisho.

**Kielelezo 2.2**

2. Karama alikuwa ni mtu mmoja ~~maarufu~~ ~~sana~~ aliyepata umaarufu ghafla katika kijiji cha Kuradikita. Kati ya wanakijiji wa Kuradikita, wapo ambapo walimchukulia Karama kama mtu bora mwenye juhudi ambaye hana mfano wake, na wapo ambao wanasema Karama ni mjinga aliyekuwa akicheza na hatari kubwa iliyokuwa taya mbele yake.

Watu ambao walikuwa wakimwona ni mwenye juhudi walijawa na wasiwasi na waliokuwa wakimchukia walikuwa na furaha. Hata hivyo hakuna aliyethubutu kusema wazo lake.

Karama alijitahidi kadri alivyoweza kujitetea na kusema kwamba watu wanaoteswa ndio wanaoyajua makao yao. Uchaguzi ulikuwa ukikaribia lakini mathibitisho ya matokeo ya ujumbe hayakutangazwa.

Wajumbe waliadhibiwa vibaya mno. Kitu kilicho kifa marunguno Kuradikita na watu kutoroshi na amani.

Serikali ilitumbua juu chini kupanga ujumbe mwengine. Basi mjumbe wa tatu alijitokeza Kabuli; alikuwa ni mwenye kuchekesha, haya na busara vilevile. Kabuli alijitahidi kadri awezavyo kuikomboa Kuradikita, na japo mengi yalimkabili, ~~alipambana~~ alipambana nayo. ~~kama~~ mithili ya ngao.

Wakubwa wawili Fadhili na Burhani walitoa mchango mkubwa tu ambao unaweza kuleta maendeleo humo Kuradikita. Huko kusini kunajulikana ~~na~~ kuwa ni baridi lakini Kabuli alijitahidi kadri aliyoweza kunyanyua Kuradikita. Ali istiqa kumalizwa mara mbili mahabusu.

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyezingatia kanuni za uandishi.

## 2.2 Sehemu B: Sarufi na Utumizi wa Lugha

### 2.2.1 Swali la 3: Utata katika Mawasiliano

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na lililenga kupima matumizi ya maarifa aliyopata mtahiniwa katika ujifunzaji wa mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano*. Swali lilimtaka mtahiniwa afafanue utata uliopo katika sentensi 5 alizopewa na kwa kila sentensi alitakiwa kutoa maana mbili (2). Swali lilikuwa na jumla ya alama 05, hivyo kila maana ya tungo ilibeba alama 00½.

Swali lilijibiwa na watahiniwa wengi yaani asilimia 94 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 64.5 ya watahiniwa ndio waliojibu swali kwa usahihi. Miongoni mwao asilimia 44.3 walipata alama $01^1/_2$ hadi $02^1/_2$, kwani waliweza kufafanua utata uliokuwepo katika baadhi tu ya sentensi walizopewa. Aidha, asilimia 20.2 waliweza kufafanua utata katika idadi kubwa ya sentensi kwa usahihi na walipata alama 03 hadi $04^1/_2$. Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua kwa usahihi utata katika sentensi alizopewa.


**Kielelezo 3.1**

| | |
|---|---|
| 3 | (a) Pango |
| | – Pango ni sehemu wanyama wanapoishi. |
| | – Pango ni kama bela ambayo mtu analipa ili aweze kupata chumba. |
| | |
| | (b) barabara |
| | – Ni njia inayotumika na watu au wanapitia watu na magari. |
| | – barabara ni sawasawa yaani kuweka kitu vizuri. |
| | |
| | (c) Ali mpigia |
| | – Ni kitendo cha kuchukua kitu na kumpiga mtu fulani mfano fimbo. |
| | – Mtu fulani alipigiwa ngoma na mtu mwingine. |
| | |
| | (d) fomu |
| | – Ni karatasi ambazo huandikwa maneno. |
| | – Ni kifaa cha kukalia. |
| 3 | (e) Anaunda |
| | – Ni kama kutengeneza kitu fulani. |

Kielelezo 3.1 kinaonesha jinsi mtahiniwa alivyoweza kuonesha utata katika tungo alizopewa, kutoka kipengele (a) hadi (d), mtahiniwa huyu hakujibu kipengele (e) kwa ukamilifu, alitoa maana moja badala ya mbili.

Asilimia 35.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 01. Miongoni mwao asilimia 14.9 walipata alama 0, kwa kuwa walishindwa kufafanua utata katika sentensi walizopewa na wengine walijibu kinyume na matakwa ya swali. Mtahiniwa mmoja badala ya kuonesha utata katika sentensi alizopewa, aliuliza maswali kwa kila sentensi. Rejea Kielelezo 3.2.

**Kielelezo 3.2**


3. a) Mama Utata uliopo hapa ni kwamba Pango
- Mama anafurahia pango-limekuaje?
b) Mwalimu analima barabara kuna utata kwa sababu
barabara - ailimwi
c) Alimpigia ngoma hapana mubusika alimpigia ngo-
ma nani? uo ni utata
d) Kijana amepata fomu ya nini?
e) Baba anaunda anaunda nini?


Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye badala ya kuonesha utata wa kila sentensi aliyopewa aliuliza swali kwa kila kipengele (a) hadi (e).

### 2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno

Swali hili lilitokana na mada ya *Aina za Maneno* na lililenga kupima matumizi ya ujuzi alioupata mtahiniwa katika kubaini aina mbalimbali za maneno. Swali lilikuwa na vipengele (a) hadi (e) na lilimtaka mtahiniwa kutumia neno ‘paa’ kwa kutunga sentensi zitakazowezesha neno “paa” kuunda dhana ya nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na shamirisho. Kila kipengele kilikuwa na alama 01 na swali zima lilikuwa na jumla ya alama 05.

Swali lilijibiwa na asilimia 92.1 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Asilimia 45.8 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 01, miongoni mwao asilimia 20.6 walipata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kabisa kutumia neno paa katika sentensi kubainisha dhana walizoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alinyumbua neno paa badala ya kutumia neno hilo katika sentensi ili kuunda dhana mbalimbali. Rejea Kielelezo 4.1.


**Kielelezo 4.1**


a/ panga
b/ paangalia
c/ paangazia
d/ paangalizi
e/ paa nanzi

Kielelezo 4.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutumia neno ‘paa’ kuunda dhana mbalimbali badala yake alinyumbua neno ‘paa.’

Asilimia 54.2 ya watahiniwa walijibu swali hili kwa usahihi, miongoni mwao asilimia 28.3 walipata alama $01\frac{1}{2}$ hadi $02\frac{1}{2}$ kwa kuwa waliweza kutumia neno ‘paa’ kuunda baadhi ya dhana na walishindwa baadhi ya vipengele. Asilimia 25 walipata alama 03 hadi $04\frac{1}{2}$ kwa sababu waliweza kuunda idadi kubwa ya dhana na kushindwa chache sana. Aidha, asilimia 0.9 waliweza kuunda dhana zote hivyo kupata alama zote 05. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuunda dhana zote tano kwa usahihi.

**Kielelezo 4.2**


4 (a) Paa la nyumba yetu limengoka
(b) Ndege mtini umepaa angani
(c) Paka yu paani
(d) Nyumba ya paa hutumia kuliko ya nyasi
(e) Upepo umevunja paa lile chakavu


Kielelezo 4.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa majibu sahihi kwa vipengele vyote (a) hadi (e).

### 2.2.3 Swali la 5: Uundaji wa Maneno

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* kipengele cha uambishaji na lililenga kupima maarifa aliyoyapata mtahiniwa. Swali lilikuwa na vipengele (a) hadi (j) na lilimtaka mtahiniwa kubaini mzizi wa asili kwa kila neno alilopewa. Swali lilikuwa na jumla ya alama 05.

Swali hili lilijibiwa na idadi kubwa ya watahiniwa yaani asilimia 94.5. Hata hivyo asilimia 58.7 ya watahiniwa walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi. Watahiniwa hao walishindwa kubaini mzizi wa asili wa maneno waliyopewa na wengine hawakuelewa kabisa matakwa ya swali hivyo walipata alama 0 hadi 01, miongoni mwao asilimia 22.1 walipata alama 0. Kwa mfano mtahiniwa mmoja badala ya kuonesha mzizi wa neno alionesha alama za kategoria za kila neno. Rejea Kielelezo 5.1.

**Kielelezo 5.1**



5 (a) N
(b) T
(c) V
(d) N
(e) E
(f) K
(g) N
(h) E
(i) E
(j) N

Kielelezo 5.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali, badala ya kubainisha mzizi wa asili kwa kila neno aliandika alama za kikategoria za maneno aliyopewa. Hata hivyo hakuwa sahihi katika matumizi ya alama hizi, kwa mfano kipengele (a) neno ambalo ni kitenzi alama yake ya kategoria ni 'T' lakini mtahiniwa aliandika 'N' yaani nomino hali inayodhihirisha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sarufi ya lugha.

Asilimia 41.3% tu ya watahiniwa ndio waliojibu swali hili vizuri. Miongoni mwao asilimia 27.4 waliweza kuonesha baadhi tu ya mizizi ya asili ya maneno waliyopewa hivyo kupata alama $01^{1}/_{2}$ hadi $02^{1}/_{2}$. Aidha, asilimia 13.8 waliweza kwa kiasi kikubwa kubainisha mizizi ya asili ya maneno waliyopewa na kupata alama 03 hadi $04^{1}/_{2}$. Watahiniwa walioweza kubainisha mizizi ya asili ya maneno na kupata alama zote 05 walikuwa asilimia 0.1. Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuonesha mizizi ya asili ya maneno yote aliyopewa.

**Kielelezo 5.2**

5 (a) Anawaandikisha
A-na-wa-andik-ish-a
Mzizi wa neno Anawaanikisha ni -andik-

(b) Mkimbizi
M-kimbi-zi
Mzizi wa neno mkimbizi ni kimbi-

(c) Mlaji
M-l-a-ji
Mzizi wa neno mlaji ni l-

(d) Muumbaji
Mu-~~u~~mb-aji
Mzizi wa neno Muumbaji ni umb-

(e) Nisingelipenda
Ni-si-nge-li-pend-a
Mzizi wa neno nisingelipenda ni pend-

(f) Kuburudika
Ku-burud-ik-a
Mzizi wa neno kuburudika ni burud-

(g) Sadifu
Sadif-u
Mzizi wa neno sadifu ni sadif

(h) Aliokota
A-li-okot-a
Mzizi wa neno aliokota ni -okot-

5 (i) Walichopoka
Wa-li-chopok-a
Mzizi wa neno walichopoka ni chopok-

(j) Kipambanuliwe
~~Ki-pa-m~~ Ki-pambanu-liwe
Mzizi wa neno kipambanuliwe ni pambanu-


Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kubainisha mzizi wa asili kwa kila neno alilopewa.

### 2.2.4 Swali la 6: Uundaji wa Maneno

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* kipengele cha uambishaji. Swali lililenga kupima maarifa aliyoyapata mtahiniwa kuhusu uambishaji wa maneno ya Kiswahili. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubadili vitenzi alivyopewa kuwa katika kauli ya kutendeka. Swali hili liligawanyika katika vipengele (a) hadi (j) na kila kipengele kilibeba alama 00½, hivyo kufanya swali zima kuwa na jumla ya alama 05.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na idadi kubwa ya watahiniwa yaani asilimia 96.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Asilimia 66.8 walijibu swali hili kwa usahihi. Miongoni mwao asilimia 8.9 walipata alama $01^{1}/_{2}$ hadi $02^{1}/_{2}$, kwa sababu walibadili kwa usahihi baadhi ya vitenzi na kushindwa vingine. Asilimia 48.8 walipata alama 03 hadi $04^{1}/_{2}$, kwa kuwa waliweza kubadililisha vitenzi vingi kwa usahihi. Aidha, asilimia 9 ndio waliopata alama zote 05, kwa sababu waliweza kuvibadili kwa usahihi vitenzi vyote walivyopewa. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebadili vitenzi vyote kwa usahihi.

**Kielelezo 6.1**




| | |
|---|---|
| 6a) | Badilika. |
| b) | Katika |
| c) | Kombeka |
| d) | Zuilika |
| e) | Tikika. |
| f) | Zoleka |
| g) | Jengeka |
| h) | Rembeka |
| i) | Tumika. |
| j) | Limika. |

Kielelezo 6.1 kinaonesha mtahiniwa aliyeweza kuvibadili vitenzi vyote alivyopewa na kuviweka katika kauli ya kutendeka.

Aidha, asilimia 33.2 ya watahiniwa walishindwa kubadili vitenzi walivyopewa kuwa katika kauli ya kutendeka, hivyo walipata alama 0 hadi 0.1. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye badala ya kubadili vitenzi alivyopewa kuwa katika kauli ya kutendeka, aliandika kinyume cha vitenzi alivyopewa.

**Kielelezo 6.2**



Kielelezo 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye aliandika kinyume cha vitenzi alivyopewa kwa mfano kitenzi ‘jenga’ aliandika kinyume chake ambacho ni ‘bomoa,’ badala ya kubadili vitenzi kuwa katika kauli ya kutendeka.


### 2.2.5 Swali la 7: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* hususan mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi* na lililenga kupima maarifa aliyonayo mtahiniwa katika kutumia kamusi. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze maana tano za neno ‘chenga’ kwa kutumia sentensi tano tofauti. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 05.

Asilimia 90.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Licha ya kujibiwa na idadi kubwa ya watahiniwa, swali hili pia ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 75.9 ya watahiniwa walijibu swali hili kwa usahihi. Miongoni mwao asilimia 28.7 walipata alama $01^{1}/_{2}$ hadi $02^{1}/_{2}$, kwa kuwa waliweza kutunga baadhi ya sentensi na kushindwa zingine. Asilimia 46.1 waliweza kuandika idadi kubwa ya sentensi kwa usahihi na walipata alama 03 hadi $04^{1}/_{2}$. Aidha, asilimia 1.1 ya watahiniwa walipata alama zote 05. Kielelezo 7.1

kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetunga sentensi zote kwa usahihi.


**Kielelezo 7.1**


7 (i) Chenga wa bahari ni mtamu sana
(ii) Bakari alimchenga baba yake shamba-ni
(iii) Mwajuma alipeta chenga za mchele
(iv) Ally alichenga kuni
(v) Mchezaji alimchenga golikipa

Kielelezo 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili katika vipengele vyote.

Watahiniwa wachache (24.1%) walishindwa kutoa majibu sahihi ya swali hili na walipata alama 0 hadi 01. Watahiniwa hao hawakuweza kutumia neno ‘Chenga’ katika sentensi tano tofauti. Kielelezo kifuatacho ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili badala ya kutumia neno ‘Chenga’ alitumia neno ‘Changa.’

**Kielelezo 7.2**


7: Kufafanua maana ya neno Changa kwa kutumia sentensi tano tofauti
(i) Tunachanga mchango wa sherehe
(ii) hapa barabarani kuna changa-jingi sana.
(iii) Kuchanga kalata.
(iv) Kuchanga kamma kitendo cha kutoa kitu fulani

Kielelezo 7.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutumia neno “Chenga” na akatumia neno “changa” katika sentensi.

## 2.3 Sehemu C: Uandishi

### 2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Insha

Swali hili lilihusu mada ya *Uandishi* katika kipengele cha *Uandishi wa Insha*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa

katika uundaji wa mawazo. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika insha ya maneno yasiyopungua mia mbili (200) na yasiyozidi mia tatu (300) kuhusu methali isemayo “Samaki mkunje angali mbichi” na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Watahiniwa walipaswa kuzingatia mambo kadhaa katika uandishi wa insha hiyo, kama vile; kuandika *kichwa cha habari kwa herufi kubwa na kukipigia mstari, kufafanua methali waliyopewa katika utangulizi, kuhakikisha kuwa kiini cha insha kina aya zenye hoja zinazoendana na methali waliyopewa, kuhakikisha kuwa mwisho wa insha una maoni na mapendekezo, kuzingatia matumizi ya alama na vituo (mfano nukta, koma, nukta mbili n.k), matumizi ya lugha sanifu na kuzingatia idadi ya maneno.*

Swali lilijibiwa na asilimia 51.8 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 83.7 ya watahiniwa hao walijibu swali hili vizuri, miongoni mwao asilimia 44.6 walipata alama kati ya 03 hadi $05^1/_2$, kwa kuwa walizingatia baadhi tu ya taratibu za uandishi wa insha. Asilimia 38.5 walipata alama 06 hadi $09^1/_2$ kwa kuwa kwa kiasi kikubwa walizingatia taratibu za uandishi wa insha. Aidha, ni asilimia 0.1 tu ndio waliozingatia taratibu zote hivyo walipata alama zote 10. Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefuata taratibu zote za uandishi wa insha.

**Kielelezo 8.1**

8 SAMAKI MKUNJE ANGALI MBICHI

Maana ya methali hii ni kumrekebisha mtoto tabia mbaya ili baadae asiendelee nazo kwani akizoea haziachi ataendelea nazo na hawezikani kurekebishwa tena. Ni msemo mzuri sana tunaoutumia ili kumuamsha au kumkumbusha mlezi kumlea mtoto vizuri Methali hii ina faida zifuatazo.

Kumuepusha mtoto na madhara ya tabia mbaya, ikiwa mtoto atarekebishwa kabla basi huepuka mambo mbalimbali kamavile wizi, ulevi uvutaji sigara.

Kumpa mlezi au mzazi angalizo, mwongo kumlea mtoto huhamasishwa na msemo huu katika kumlea mtoto katika maadili mema. Mtoto anapofunzwa tabia njema basi msemo huo umefanikiwa katika kumjenga mtoto.

Kupata kizazi kizuri, watoto wanapofunzwa tabia njema mapema basi jamii huwa yenye kujitambua na kufanya mambo ya kimaendeleo mfano bidii katika kazi, kusaidiana, kutafuta elimu na kuwaheshimu watu wote hivyo kizazi kinaendelea kuwa kizuri

Huleta maendeleo, vilevile methali hii hutumiwa katika kumuandaa mtoto kukabiliana na changamoto za maisha ambapo ni chanzo cha maendeleo.

Vilevile methali hii isipotumiwa katika kumjenga mtoto kitabia huleta madhara mbalimbali katika jamii. Yafuatayo ni madhara au hasara za kutotumia methali hii

8 Mtoto kuwa na tabia mbaya, mfano wizi, lugha chafu, uzembe, uvivu na kutokuwa na heshima. Mtoto asipofunzwa tabia nzuri huwa na tabia mbovu hivyo tunakuja. Samaki angali mbichi kwani akikauka hakunjiki tena

Kizazi kibaya, pia tunakuwa na kizazi kisicholeta maendeleo kwani huwa hawajishughulishi na mambo ya kuleta maendeleo.

Huleta umasikini, ikiwa mtoto hajapatiwa tabia njema kabla hushindwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuishi maisha ya kutegemea wengine tu mfano Mwizi.

Kwa kumalizia, hatunabudi kuwapatia watoto tabia njema wangali hawajakuwa ili waendelee nazo.

Kielelezo 8.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kuzingatia taratibu sahihi za uandishi wa insha.

Watahiniwa wachache tu (16.3%) ndio ambao hawakuzingatia taratibu za uandishi wa insha, hivyo walipata alama 0 hadi $02^1/_2$. Miongoni mwao, wapo walioandika hadithi badala ya insha, wengine waliandika habari bila kuweka hoja katika aya na pia hawakutumia alama za uandishi. Mtahiniwa mmoja badala ya kuandika insha alitunga hadithi ambayo ni ya kipera cha 'ngano.' Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika hadithi badala ya insha.

**Kielelezo 8.2**

| | |
|---|---|
| 8 | SAMAKI MKUNJE ANGALI MBICHI |
| | Hapo zamani za kale palitokea mtoto. mtukutu aliyekuwa anaitwa |
| | Jonaji. Mtoto huyu alikuwa anaishi na wazazi. wake walioitwa mzee |
| | Komba na bibi Magumashi. Mzee Komba na bibi Magumashi walimpenda |
| | sana Jonaji. Wazazi hawa kamwe hawakuwai kumwadhibu mtoto wao |
| | alipokuwa akifanya makosa huku wakidai kuwa akiwa mkubwa ataacha |
| | utukutu na kuwa kijana mstaarabu. |
| | Familia ya mzee Komba iliishi maisha ya dhiki sana. Kuna wakati |
| | familia hii ilikosa kula na kulazimika kulala hivyo hivyo. Mzee Komba |
| | alikuwa ni mlevi kupindukia hali kadhalika bibi Magumashi nae. |
| | Siku moja mzee Komba alienda kwa kaka yake mzee Simba. |
| | Alipofika kule mzee Komba alimkuta kaka yake anamwadhibu mwanaye. |
| | Mzee Komba alianza kumlaumu kaka yake kwa kumwadhibu mtoto huku |
| | akidai kuwa watoto hawatakiwi kuchapwa wala kuraripiwa bali wanat |
| | akiwa kusamehewa na wakikua wataacha utukutu Mzee simba alimwam |
| | bia ndugu yake kuwa watoto wanapaswa kupata mafunzo na kupewa adhabu |
| | pale inapostahili. Mzee Komba alicheka sana na kuanza kumuita kaka |
| | yake kuwa yeye ni mjinga. Lakini kwa kuwa mzee Simba anaijua tabia |
| | ya dharau ya ndugu yake alinyamaza kimya. |
| | Baada ya miaka mingi kupita Jonaji alikua kijana mkubwa. |
| | Alianza kulewa kama wazazi wake na akawa anawaibia watu pale kijijini |
| | Wananchi wenye huruma walimwambia mzee Komba amkanye mwanae |
| | lakini mzee Komba kila alipomkanya mwanaye, Jonaji hakuacha tabia ya |
| | ke ya wizi. Siku moja Jonaji aliiba runinga na bahati mbaya zaidi |
| | alikamatwa. Watu kwa hasira walimpiga alafu wakamchoma moto. |
| | LOOOO! Kwa masikitiko makubwa mzee Komba na mkewe walili |
| | a sana walipoona mwanawe akiteketea kwa moto. Ndipo kwa sauti kali |
| | Mzee Komba alisema, "Ama kweli Samaki mkunje angali mbichi." Watu |
| | walimwambia kuwa tatizo alishindwa kumdhibiti mwanae tangu utotoni |
| | na matokeo yake akachomwa moto. |

Kielelezo 8.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika 'ngano' badala ya insha.

### 2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Hotuba

Swali hili lilihusu mada ya *Uandishi* katika kipengele cha uandishi wa hotuba na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuunda mawazo. Swali lilimtaka mtahiniwa ajifanye Mwenyekiti wa mtaa wa Kwamachombo, ambao umekumbwa na mafuriko na atoe hotuba ya kuwashawishi wananchi hao ambao wamekataa kuhama, ili waweze kuhamia makazi mapya ya Kitivo. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10.

Katika uandishi wa hotuba watahiniwa walitakiwa kuzingatia yafuatayo: *salamu, utambulisho, kiini cha hotuba chenye aya zilizo na hoja zenye mantiki, hitimisho, matumizi ya alama za uandishi (mfano, nukta, koma, nukta mbili n.k) na matumizi ya lugha sanifu.*

Swali lilijibiwa na asilimia 38.7 tu ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 89.7 ya watahiniwa hao walijibu swali hili kwa usahihi ambapo miongoni mwao asilimia 49.6 walipata alama 03 hadi $05^1/_2$ kwa kuwa walikiuka baadhi ya taratibu za uandishi wa hotuba. Aidha, asilimia 40 walipata alama 06 hadi $09^1/_2$, kwa kuwa kwa kiasi kikubwa walifuata taratibu za uandishi wa hotuba. Watahiniwa waliozingatia kanuni zote za uandishi wa hotuba ni asilimia 0.1, hivyo walipata alama zote 10. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyezingatia kanuni za uandishi wa hotuba.

**Kielelezo 9.1**

9\. HOTUBA KWA WAKAZI WA KIMACHOMBO

Wananchi oyooo! Kwamachombo oyooo!
Nina imani kuwa kila mmoja wenu yuko salama kiafya na katika maendeleo binafsi, au sio! Ndugo zangu wananchi, napenda kuwapa pole sana kwa majanga ya mafuriko yanayotokea! Nina imani nyote mmeshapoa.

Kama mnavyojua eneo letu la Kwamachombo linakumbwa sana na mafuriko ambayo yanaharibu kwa sana katika maendeleo yetu hasa katika sekta ya kilimo na ujenzi wa Mashule na barabara, hivyo basi, mimi Mwenyekiti ninapenda kuwapa ushauri wa bure tu! kwamba ni bora

a tuhamie eneo lingine lisilo na maafuriko wala migogoro yoyote. Na eneo hilo si lingine bali ni kitivo.

Ndugu zangu wananchi, eneo hili lina vitu vingi vizuri kama ardhi iliyosheheni rutuba na maji ya kutosha kulingana na eneo hili la Kwamachombo. Bila shaka mtapapenda kwa ardhi na mchanga hata usiohitaji mbolea kwani ni mzuri.

Pia, ndugu zangu kitivo pana ziwa kubwa lililosheheni samaki wa aina nyingi ambao kama ninavyojua mwapenda sana uvuvi! au sio! hivyo basi hatuna budi tuhamie huko ili kuendeleza kazi ya uvuvi zaidi na kwa faida.

Mtaa wetu wa Kwamachombo hauna soko la kuuza bidhaa zetu, mazao na samaki lakini kitivo! ambadanganya mtu! kuna soko kubwa sana ambalo bila shaka tutafaidika tukiishi pale kwani wauzaji ni wachache na wanunuaji ni wengi! hiyo ni raha, au sio ka raha?

Mwezi uliopita nilishuhudia mwenyewe Shule kumi na mbili na barabara zikijengwa - kwa maana hiyo kitivo hakuna shaka wa uhaba wa shule za kuwapeleka vijana wetu! Vijana ~~Mtaa~~ mtahama! au la! Shule ni zenu!

Bila kusahau janga kuu! kitivo hakuna Maafuriko wala dalili zozote za janga lolote, Eneo hilo lina hewa nzuri, mvua za kutosha, jua shwari na upepo wa ziwani! Kweli ndugu Wananchi ningependa sana kuwasihi mkitaka kuhamia kitivo maana hakuna shaka wa kitu chochote

a. ~~H~~ Hivyo ndugu wananchi wa mtaa wa Kwamachombo sina budi kusema asante kwa kunisikiliza na ninaamini mnamo mwezi ujao sote tutaitwa Wananchi wa mtaa wa kitivo! Kitivo oyeee! kitivo oyeee! haya! Mungu awabariki nyote.

Kielelezo 9.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kuzingatia muundo wa hotuba.

Asilimia 10.3 tu ya watahiniwa ndio walioshindwa kuandika hotuba kwa kuzingatia taratibu za uandishi. Watahiniwa hao

walipata alama 0 hadi $02^1/_2$ kati ya alama 10. Miongoni mwao wapo walioandika hadithi, wengine waliandika habari yenye mfululizo usiokuwa na aya. Mtahiniwa mmoja aliandika barua ya kikazi kwa mheshimiwa Diwani akiomba kuhamia makazi mapya eneo la Kitivo. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa huyo.

**Kielelezo 9.2**

9

KWA MWACHOMBO,
S.L.P 447,
Mbeya
12/2004,

~~MH: DIWA~~

MH: DIWANI
S.L.P 432
ISUMP. MBEYA
20/10/2004

YAH:
MAOMBI YA KUHAMIA MAKAZI MAPYA ENEO KITIVO.

Naomba kusikia na kichwa cha hapo juu mimi ni mwenyekiti wa mta wa mwachombo, ndugu wananchi wa mta wa kwa mwachombo ninayofuraha kubwa kutarifu kwa inabidi tuhame kwenye mta wetu hu kwa sababu tifurataro mta a ukosehemu mbaya mayo kutoka a mt mtaturiko mara kwa mara hivyo basi itabidi tuhame kabla hatuja kumbana nayo, ndugu mhemiwa ombi letu letu ushugulikiwe

Ni mimi mtiifu,
mwenyekiti wa mtaa
M. mtaa,

Kielelezo 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika barua ya kikazi badala ya hotuba. Hata hivyo mtahiniwa huyo anaonesha kuwa hana ujuzi wa uandishi wa barua za kikazi kwa sababu aliandika tarehe sehemu ya anwani ya mwandikiwa wa barua hiyo, hivyo kufanya barua yake kuwa na tarehe mbili.

## 2.4 Sehemu D: Maendeleo ya Kiswahili

### 2.4.1 Swali la 10: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili

Swali hili lilitoka kwenye mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uchambuzi wa maarifa aliyopata kuhusu namna utawala wa Waingereza ulivyoimarisha Kiswahili nchini Tanzania kwa kupitia mfumo wa elimu. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10.

Asilimia 87.6 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili, kwa sababu lilikuwa swali pekee katika sehemu D. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya na idadi kubwa ya watahiniwa, kwani asilimia 66.1 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi $02^1/_2$, miongoni mwao asilimia 25.3 walipata alama 0. Baadhi ya watahiniwa waliandika Taasisi zinazokuza na kueneza lugha ya Kiswahili, wengine walionesha shughuli mbalimbali za Waingereza katika utawala wao kama vile dini, utawala na uundaji wa taasisi za usanifishaji wa lugha. Watahiniwa hao hawakuonesha jinsi mfumo wa elimu katika kipindi cha utawala wa Mwiingereza ulivyoimarisha Kiswahili. Kielelezo 10.1 kinaonesha mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo 10.1**

10 Kiswahili nchini Tanzania kimewera kuimarisha na utawala wa Waingereza kwa kutumia hoja zifuatazo ambazo zimewera kuimarisha Kiswahili.

BAKITA Baraza a kiswahili nchini Tanzania ambalo limewera kusaidia kiswahili kiwere kudumu na kuimarika wa sababu BAKITA ni baraza ambalo linahifadhi uwelewa wa kiswahili na kuwera kutunga mtihani pamoja na kuweka kumbukumbu kwa ajili ya kuimarisha kiswahili nchini Tanzania.

TUKI ni taasisi ya Uchunguzi wa kiswahili ambayo linawera kuchunguza kuwa kiswahili kinaendelea kifasaha na na kuwere kuimarika katika nchi pamoja na ushirikiano baina ya watu na viongozi wanaoshughulikia na suala la kiswahili nchini Tanzania. Pia tuki huwera kusaidia na kuimarisha jamii katika uchunguzi huu wa kila siku ambao unawera kusaidia kiswahili kuenea katika bara hili la Tanzania.

BAMITA ni baraza la mtihani Tanzania ambalo linashughulikia masuala la mtihani kwa mtihani umeonyeshwa au mtihani haujaonyeshwa na pia kazi nyingine ambayo BAMITA anashughulikia ni kuwepo kwa wasimamizi ambao hawaweri wakaonyesha mtihani wala kuwapa watu ambaowanafasha mtihani majibu ambayo watawere kuwa miongo-

ni mwa wale watu ambao wamekiuka amri za Mungu na kuweza kuchukuliwa sheria na kupewa adhabu kwa sababu watu hao wameweza kuonyesha mtihani ndiyo maana bamita inaweza kusimamia watu hao ili wasijeweza kuonyesha mtihana na BAMITA inawaogocha watu hao ambao wanasimamia mtihani huo.

CHAKA ni chama cha Kiswahili Afrika ambacho kinaweza kushirikiana na vyama vingine ili kuweza kuendeleza Kiswahili nchini Tanzania na kuweza kudumisha Kiswahili kwa lengo la kuwa mtu ambaye anaweza kuleta maendeleo ya Kiswahili kupitia chama cha Kiswahili Afrika.

UWAVITA ni umoja wa vikundi vya Kiswahili Tanzania ambao unaweza kushikamana kwa ajili ya kuimarisha Kiswahili kwa lengo la kuwa na maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania.

Hivyo basi Waingereza waliweza kuimarisha Kiswahili nchini Tanzania kwa kupitia mfumo wa Elimu ambao ni TUKI BAKITA BAMITA UWAVITA CHAKA na wametumia mbinu nyingi kwa ajili ya kuimarisha Kiswahili nchini Tanzania.

Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika Taasisi zinazokuza lugha ya Kiswahili badala ya kuonesha jinsi mfumo wa elimu kipindi cha Mwiingereza ulivyoimarisha lugha ya Kiswahili. Aidha, Taasisi alizotaja zingine hazikuwepo kipindi cha utawala wa Mwiingereza. Kwa mfano taasisi kama BAMITA, CHAKA na UWAVITA.

Asilimia ndogo (33.9%) ya watahiniwa waliweza kujibu swali hili kwa usahihi. Miongoni mwao asilimia 25.4 walipata alama 03 hadi 05½, kwa kuwa waliweza kueleza kwa kutumia hoja chache kuhusu jinsi mfumo wa elimu wa Mwingereza ulivyosaidia kuimarisha Kiswahili. Aidha, asilimia 8.5 ndio waliopata alama 06 hadi 09½ kwa kuwa waliweza kutumia hoja nyingi kufafanua jinsi utawala wa Waingereza ulivyoimarisha Kiswahili nchini Tanzania kwa kupitia mfumo wa elimu. Kielelezo 10.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 10.2**

| | |
|---|---|
| 10. | Ni kweli kwamba waingireza wameimarisha |
| | kiswahili ~~kth~~ kupitia Mfumo wa elimu kama navyo |
| | thibitisha kama itakavyo. |
| | Kuchapisha vitabu vingi vya kiswahili. Waingere |
| | za waliweza kuimarisha Kiswahili kwa kuchapisha |
| | vitu vya kiswahili kwa wingi na hatimaye Kiswahili |
| | kilienea na kuimarika kwa haraka zaidi. |
| | Kuchapisha ~~kamusi~~ ~~ya~~ za kiswahili. Pia uchapi |
| | shaji wa kamusi za kiswahili kilisaidia kukua na |
| | kuenea kwa kiswahili nchini Tanzania kwa |
| | kuchapisha kamusi za kiswahili nchini |
| | Kufundishwa kwa kiswahili kama somo shuleni. Pia |
| | Kufundishwa kwa kiswahili kama Somo mashuleni |
| | enzi za waingereza ilisaidia kuimarika kwa lugha |
| | ya kiswahili enzi za waingereza. |
| | Kuundwa kwa kamati kuu mayosimamia kiswa |
| | hili. Enzi za mfumo wa elimu wa waingereza |
| | waliimarisha lugha ya kiswahili kwa kuunda |
| | ~~camate~~ kamati iliyo kuwa inasaidia katika usanifisha |
| | ji wa kiswahili nchini Tanzania. |
| | ~~Kuwalazimisha~~ Kutumia lugha ya kiswahili katika |
| | ufundishaji wa Masomo Shuleni. Pia kitu kingine |
| | Kilichoimarisha kiswahili enzi za uingereza katika |
| | ngazi ya kutoa elimu ilikuwa ni kutumika kwa |
| | kiswahili kama lugha kuu katika kufundishia mashu |
| | leni na hiyo ilisaidia kuimarisha Kiswahili. |
| | Nahitimisha kwa kusema hizi ambazo zipo |
| | hapo juu ni vitu ambavyo vilichangia kwa |
| | kiasi kikubwa kuimarika kwa kiswahili |
| | katika Mfumo wa elimu enzi za wainger |
| | za na siyo katika mfumo huo tu bali katika |

Kielelezo 10.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyefafanua jinsi utawala wa Waingereza ulivyoimarisha Kiswahili nchini Tanzania kwa kupitia mfumo wa elimu.

## 2.5 Sehemu E: Fasihi kwa Ujumla

### 2.5.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kufanya tathmini ya ujumbe wa methali. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia methali sita katika kuthibitisha hoja kuwa, kutokana na mabadiliko katika jamii baadhi ya methali zimepitwa na wakati. Swali hili lilikuwa na alama 15.

Swali lilijibiwa na asilimia 28.2 tu ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 66.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu kwa usahihi. Miongoni mwao asilimia 45 walipata alama $04^{1}/_{2}$ hadi $08^{1}/_{2}$, kwa kuwa waliweza kutaja baadhi ya methali na kutoa ufafanuzi wa kuhusu methali hizo. Asilimia 21.3 ya watahiniwa walitumia idadi kubwa ya methali na kutoa ufafanuzi sahihi hivyo walipata alama 09 hadi $14^{1}/_{2}$. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali.


**Kielelezo 11.1**

11 Methali ni aina ya semi ambayo hutoa hekima na busara katika jamii. Methali kama utanzu wa fasihi simulizi umeweza kufanya kazi kubwa kama kuonya, kuadhibu, kurudisha na zaidi ya yote kuelimisha jamii. Hata hivyo kutokana na mabadiliko yanayoikumba jamii, baadhi ya methali zimepitwa na wakati na hazina tena maana katika jamii nazo ni pamoja na;

Pole ~~na~~ Haraka haraka haina baraka. Methali hii inaeleza kuwa vitu vinavyofanywa haraka mara nyingi huwa haviloti matokeo mazuri. Methali hii imepitwa na wakati kwani dunia ya siku hizi inahitaji uwe na haraka ya kufanya vitu ili uwende sambamba na maendeleo yanayo tokea katika jamii. Kwa mfano mgonjwa aliyeugua ghafla anapaswa kuharakishwa na kupelekwa hospitali kabla ya hali ya kuzorota na kuwa mbaya.

Mvumilivu hula mbivu. Methali hii inaeleza kuwa mtu anayevumilia shida na mateso kwa muda mrefu mwishoni huja kufanikiwa. Methali hii imepitwa na wakati kwani kuna mambo yanayotokea katika jamii ambayo hayavumiliki na hata ukivumilia hayaishi. Kwa mfano watu kama wakulima, wazee na maskini huvumilia shida mpaka mwisho na bado hawapati faraja yoyote wanaendelea kunyonywa na kuonewa na bakuna mkombozi wa kuwaokoa.

Pia methali ya mchumia juani hulia kivulini imepitwa na wakati. Methali hii inasema kuwa mtu anayeteseka akitafuta maisha ipo siku atafanikiwa. Katika dunia ya leo mambo ni tofauti tukichukulia mfano wa wakulima. Licha ya kazi kubwa wanayofanya bado ni maskini, kipato ni kidogo hawathaminiwi wanateseka kusaidia taifa lakini bado wananyonywa na hawaendelei



11 Methali ya heri nusu shari kuliko shari kamili imepitwa na wakati. Methali hii inaeleza kuwa bora upate kitu kidogo badala ya ~~chote~~ kukosa chote. Methali hii imepitwa na wakati kwani kuna vitu vingine huwezi kuchukua nusu ukatumia kisha ukakamilisha. Kwa mfano nguo kama gauni huwezi kuchukua sehemu ya juu ukaacha ya chini litakuwa si gauni tena hii kutokana na maendeleo ya jamii na upelevu wa muda kuenda kuhitaji kitu nzima ya pili badala ya chote.

Methali ya mtaka yote hukosa yote mwenda pole hula tende pia imepitwa na wakati. Methali hii inaeleza mtu anayefanya vitu anavyoamua atakuja siku kujutia. Kutokana na maendeleo katika jamii ya dunia ya leo mambo mengi yanayofanywa kwa si ya kweli na ni heri kuyapuuzia kwani huyaletesha na kupoteza muda. Kwa mfano pale mtu anaposhauriwa asiende shule na marafiki zake si kweli akikataa atakuja kujutia bali ni upotoshaji tu.

Mgagaa ~~bali~~ ~~wa~~ na upwa hali wali mkavu. Methali hii inaeleza kuwa mtu anayejitahidi hawezi kukosa kujikimu na kuendesha kimaisha. Methali hii imepitwa na wakati kwani siku hizi kuna mambo kama rushwa, unyonyaji yanayo wadhuru wale wanaojitahidi katika maisha. Tukichukulia mfano wa wakulima licha ya kufanya kazi kwa bidii bado ndiyo watu maskini zaidi Tanzania kutokana na rushwa, ubaguzi na ukandamizaji.


Licha ya kuwepo na methali zilizopitwa na wakati zipo nyingine ambazo bado zinaendelea na kutumika katika jamii kama vile Samaki mkunje angali mbichi. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu na akiba haiozi ambazo zote zina maana katika jamii.

Kielelezo 11.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kutaja methali na kufafanua jinsi

ujumbe uliomo katika methali hizo ulivyopitwa na wakati kutokana na mabadiliko ya jamii.

Asilimia 33.7 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 04, miongoni mwao asilimia 12.5 walipata alama 0 kwani walishindwa kabisa kutaja methali hata moja. Wengine walitaja methali tu bila ufafanuzi wowote na wengine walitaja vitendawili na kutoa maana zake, wapo walioorodhesha vitendawili na methali katika majibu yao kinyume na matakwa ya swali. Aidha, majibu yao yanaonesha kuwa watahiniwa hawajui tofauti kati ya methali na vitendawili. Kielelezo 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika vitendawili na methali katika jibu lake.

**Kielelezo 11.2**


11. Methali kipera cha fasihi ambacho hutumia
Lugha ya kiufundi ili kufikisha ujumbe kwa jam.
Zifuatazo ni hadi methali mbalimbali zilizo
ohekana kupitwa na wakati nazo ni:
Kuku hufugia mibani nanasi
Upele wa babu unatoa mvuke ugali
Asiyefunzwa na mamae hufunzwa na ulimwengu
Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
Haba na haba hujaza kibaba.
Jogoo wa shamba hawiki mjini.
Haraka haraka haina baraka

Kielelezo 11.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa alichanganya vitendawili na methali ambazo hata hivyo alishindwa kutoa maana zake.

## 2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Fasihi Andishi* na lilihusu vitabu teule vya ushairi ambapo lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia vipengele vitatu vya lugha kutoka katika diwani mbili alizosoma ili

kudhihirisha kauli kuwa ustadi wa msanii hudhihirishwa na fani. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali lilijibiwa na asilimia ndogo sana (4.4%) ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Aidha, swali hili lilijibiwa vibaya na idadi kubwa ya watahiniwa kwani asilimia 75.9 walipata alama 0 hadi 4 na miongoni mwao asilimia 46.5 walipata alama 0, kwa sababu walielezea dhamira za diwani walizopewa badala ya kuonesha jinsi lugha ilivyodhihirisha ustadi wa msanii. Kielelezo 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshidwa kukidhi matakwa ya swali.

**Kielelezo 12.1**

| | |
|---|---|
| 12. | Fani: Ni kazi ya umbo la nje ya fasihi |
| | simulizi, Ustadi ni ujuzi anao kuwa nao mtu |
| | fulani katika nafsi yake |
| | Kwa kutumia diwani vifuatazo CHEKA |
| | CHEKA T.A. MVUNGI na diwani ya pili ambayo |
| | ni WASAKATONGE Mwandishi MOHAMED S. |
| | KHATIBU (DUP). Ustadi wa msanii umedhihirishwa |
| | na fani kwa kuangalia vifuatavyo:- Katika di |
| | wani ya Cheka cheka yaliyomo ni kama hivi:- |
| | Suala la Mapenzi katika shairi la |
| | Ua mwandishi amezungumzia ustadi wake kutoka |
| | na na fani kama ilivyo onekana katika ubeti |
| | 4 ukurasa 30 akisema haya: |
| | "Ua sasa limepea" |
| | "Macho wani kodolea" |
| | ni kweli kabisa sio katika shairi bali hata jamii yetu |
| | ya leo wapo watu wanaopenda wenzi wao kama vile |
| | ua linalo mea katika bustani hivyo basi kazi |

12 ya mwandishi au msanii wa shairi hili ame dhihirisha ustadi na fani.

Mwandishi ame zungumzia suala la Kupiga vita Ukoloni Mambo leo. hii ni suala la kuondoa Ukoloni katika nchi imekuwa ndio gumzo katika jamii nyingi barani Afrika ila kuto kana na mwandishi kuwa na ustadi katika Ukurasa wa 43 ubeti 8 shairi lake la Mwinyi ame zungumza haya

"Mwinyi umewasha moto
" Angalia usizime "
Ukoloni pigwa vita barani

Ni kweli kabisa hata jamii ya leo watanzania wanaishi bila kuendeshwa kikoloni kutokana na jinsi uhuru uliyo tawala nchi.

Mwandishi alizungumzia suala la rushwa ni kitendo cha kutoa au kupokea fedha au amana kwa kusudio la kupewa au kupata kitu fulani ime onekana katika shairi la Kasuku mwandishi ame dhihirisha ustadi kwa kutumia fani anapo onesha Kasuku katika ukurasa 28 bet 3. akisema " Tuambae ukasuku

wale wasopenda shiriki"
Pokea zao kurudi kuhemea "
" wengi bila fedha pipaha

hivyo kweli ustadi hudhihirika kutokana na fani katika fasihi andishi au fasihi simulizi.

Mwandishi ameonesha suala la Matabaka katika shairi la Samaki Mtungoni pale anapo sema haya katika Ukurasa 53 ubeti 4 " Samaki majini wangu"
" bila tungo shikeliza"

12 ni kweli kabisa hata jamii zetu za leo tunazoishi watu wengi huwa katika matabaka kutokana na suala la Ubinafsi

Kutokana na ustadi wa Mwandishi katika diwani ya Cheka cheka imedhihirika kutokana na fani pamoja na ustadi

Kwa kutumia diwani ya pili pia ambayo ni WASAKA TONGE Mwandishi MOHAMED KHAMIS (SUPI

Mwandishi ameonesha suala la Uongozi mbaya wa Viongozi wa dini viongozi wa dini sio waaminifu mbele za watu hata Mungu huyo tume ona haya katika shairi la WASODHAMBI katika Ukurasa 32 ubeti 1. akisema haya:-

"Wajigamba eti safi rohoni
Tashititi kwa rozari"
" Eti safi rohoni "

Ni kweli kabisa kazi ya ustadi wa mwandishi imedhihirika kutokana na fani kwani hata jamii ya leo napo viongozi walio wabaya katika dini zao.

Mwandishi ameonesha suala la Unyonyaji ni kitendo cha kumlaghai mtu au kumnyima mtu halali yake katika shairi la "wapi twendako?" katika Ukurasa 28 ubeti 4

"Magharibi siko
" Mashariki siko "
Wapi twendako
Zahimika nguvu zetu
" Bila kupata kitu

Huyo basi hata jamii za sasa vijana au watu wengi wana nyonywa ki maslahi kwani hawapewi fedha halali ya malipo ya kazi wanazofanya

12 hata hivyo kauli ya mwandishi ina dhihirika kutokana na ustadi na fani

Mwandishi amezungumzia suala la Nafasi ya mwanamke katika jamii wanawake wamekuwa wakionewa kwenye jamii nyingi hasa katika shairi la "Mwanamke wa Afrika" katika Ukurasa 33 ubeti 2 akisema haya,

" Namwona shambani
Jembe mkononi mazao sio yake "
" Yeye yaya, yeye dobi

Kwani hata sasa tunapoishi wanawake wengi wana nyanyasika katika jamii zao, katika suala la kazi hawapati muda wa kupumzika hivyo basi kazi yako mwandishi inadhihirika kwa ustadi na fani.

Suala la Mapenzi katika diwani hii mwandishi ameonesha upendo wa dhati hasa tu pale mwanamke anapo fananishwa na Njiwa kiumbe mtni" katika shairi ya "Njiwa" Ukurasa 30 ubet 3-

" Njiwa wangu
Kiumbe mti "
" Ume gubikwa kwa njozi
Wangu wa moyo"

Sio tu kwenye shairi hili bali watu wengine kwenye jamii wapo na upendo wa dhati kwa familia zao hasa wake zao

Hivyo tunapaswa kusoma kazi za wana shairi wengi ili kuchambua na kuelewa ustadi wa mambo katika jamii kwa kuzingatia ustadi nao fani kama Umbo la kazi ya nje la fasihi umulizi

Kielelezo 12.1 ni jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha jinsi lugha ilivyo nyenzo muhimu ya mwandishi katika kufikisha ujumbe, badala yake alieleza kuhusu dhamira.

Watahiniwa wachache sana (24.1%) ndio waliojibu swali hili kulingana na matakwa ya swali. Miongoni mwao asilimia 15.5 walipata alama $04^1/_2$ hadi $08^1/_2$, kwa sababu waliweza kutaja baadhi tu ya vipengele vya lugha na kuvitolea ufafanuzi. Asilimia 8.6 ya watahiniwa walipata alama 09 hadi $14^1/_2$, kwa sababu walitoa majibu sahihi yenye ufafanuzi wa kina, ingawa hawakuweza kutoa ufafanuzi kwa vipengele vyote. Kielelezo 12.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 12.2**

12. Nikweli "Ustadi wa msanii hudhihirishwa kwa fani". Na ukweli huu utadhihirishwa kwa kutumia vitabu viwili vya diwani. Nikianza na kitabu cha malenga wapya kilichoandikwa TAKILUKI kinachoelezea hasa uhusiano mbaya uliopo kati ya tabaka la juu na la chini. Vipengele vya lugha ni

Tamathali za semi, waandishi wa kitabu hiki cha diwani wanaonyesha matumizi mbalimbali ya lugha mfano Tanakali sauti na nyinginezo. Kati shairi la "mkulima" mwandishi anazema katika ubeti wa pili (2).

2. Jogoo linapowika, kokoriko mitaani
Mkulima huamka, jembe lake mkononi
Bila ya kupumzika, Huzika kwako shamba

Misemo; Misemo ni maneno ambayo yanafisha maana kuli ya maneno. Waandishi hawa wamejaribu kuielezea kipengele cha misemo katika mashairi yao mengi. Mfano katika shairi la "mwabwaja mwasema nini" ubeti wa 1. Mshairi anasema

1. Nasikia mnatunga, mwatungani washairi
Nasikia mnabonga, ukweli uliodhahiri
Nasikia mnapanga, mipango ilomizuri
Mwabwaja mwasemanini, zewapi zake athari

Mwandishi anatumia neno "bonga" kama kusema hadharani (bila kuficha)

Matumizi ya taswira Mwandishi amejaribu kutumia kitu baada ya kitu fulani. Mfano mwandishi ametumia neno "ua" kama msichana mrembo. Mwandishi anasema katika shairi la "ua" ubeti wa 3.

3. "...
Ukiliona langaa, macho walikodolea
Ua sasa limepea,
3. ... "
Ukiliona la ngaa, moyoni lakunngia
Ua sasa limepea, macho walikodolea

Tukija katika mashairi ya Chekacheka yaliyoandikwa na mwandishi mashuhuri kutoka zanzibar, MVUNGI yanayosimulia ubaya wa serikali tangu enzi za ukoloni. Mvungi amejaribu kutumia vipengele mbalimbali vya lugha kama vile;

Takriri; Ni ule ustadi wa kurudia rudia maneno katika kuandika kazi ya kifasihi. Mwandishi amelithibitisha hilo kwa shairi lake la "Moyo" linaloelezea mapenzi. Mvungi anasema.

Moyo ni mshauri, lakini umekaidi
Moyo kiburi hatari, mfano we kama radi,
Moyo mefumbata shari, unayakwepa maradi
Moyo yu mwilini mwangu, jirudi tuwe pamoja

Neno "moyo" limerudiwa katika kila ubeti.

Lugha ya picha; Pia, lugha ya picha kama moja ya kipengele cha matumizi ya lugha kimeonyeshwa na mvungi katika mashairi yake kadha wa kadha. Mfano katika shairi la "~~KIUMBE~~ NJIWA KIUMBE MTINI" mwandishi anafananisha mwanamke kama njiwa. Mshairi anasema.

"... Basi mie taabani, njiwa akitabasamu

Mafumbo; Pia mvungi amejaribu kuonesha baadhi ya mafumbo katika baadhi ya mashairi yake. Mfano; Mvungi ametumia mafumbo kama "Ukakasi na mtitio" akimaanisha vikao visivyo kuwa na maana yoyote vya viongozi wa nchi. Anathibitisha katika shairi la "TAIFA WAMELIZIKA"

"Mezikwa demokrasia, chama kimoja ndo ngao
Watu hawana nafasi kutetea nchi yao
Mawazo ya ukakasi, mawazo ya mtitio"

Mwisho kabisa; Fani ni kipengele cha umuhimu katika kazi ya fasihi. Ukiachana na ~~maa~~ fani maudhui haitakuwa na maana.

Kielelezo 12.2 kinafafanua jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri kwa kufafanua ustadi wa mwandishi katika kutumia vipengele mbalimbali vya lugha. Hata hivyo mtahiniwa alikuwa na makosa ya kiuandishi, kwa mfano katika aya ya 3 aliandika neno "anafisha" badala ya "anafikisha." Aidha, aliandika kuwa mwandishi Mvungi anatoka Zanzibar badala ya Tanzania Bara.

### 2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Fasihi Andishi* na lilihusu vitabu teule vya riwaya. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kufanya tathmini. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutumia riwaya mbili kujadili kukubalika kwa wahusika kama kielelezo halisi cha wanajamii kati ya Takadini, Maman'tilie na Brown Kwacha. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Asilimia 69.1 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili, ambapo asilimia 78.6 walijibu kwa usahihi na kupata alama nzuri. Miongoni mwao asilimia 38.4 walipata alama $04^1/_2$ hadi $08^1/_2$, kwa sababu walitoa hoja sahihi lakini ni chache katika kuelezea kukubalika kwa wahusika waliowachagua. Aidha, asilimia 40.2 ya watahiniwa walijibu vizuri swali hili na kupata alama 09 hadi 15, kwani waliweza kutoa hoja na kuzifafanua kwa usahihi zaidi. Kielelezo 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 13.1**

13. Wahusika ni watu, vitu au viumbe vinavyo
tumiwa na wasanii wa kazi ya fasihi simulizi -
katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Kwa
kutumia riwaya mbili za "WATOTO WA MAMA -
NTILIYE" iliyoandikwa na "EMMANUEL MBOGO"
na riwaya ya "JOKA LA MDIMU" iliyo andikwa
na "ABDALLAH SAFARI" zimejaribu kutumia -
wahusika "Mama ntiliye kutoka katika riwaya
ya "WATOTO WA MAMANTILIYE" na Brown kwacha kutoka katika
riwaya "JOKA LA MDIMU" kuonesha uhalisia wao wa uhusika
kwa kulinganisha na hali halisi ya sasa. Kwa kuan
za na riwaya ya "WATOTO WA MAMA NTILIYE" ime
mtumia muhusika mama ntiliye katika kuakisi
hali halisi ya jamii nzima na matendo yake, zifu
atazo ni hoja tatu zinazo onesha uhusika wa mu
husika huyu ambazo ni matukio halisi katik
a jamii yetu;

13. Mchapa kazi; Katika riwaya hii, mwandishi
anaonesha jinsi mama ntiliye anavyo jituma
katika kufanya kazi na biashara ndogondogo-
ambazo zitamsaidia kuingiza kipato kwa ajili
ya mahitaji ya familia yake. Pia katika jamii
yetu ya sasa wata wapo wakina mama wanao
jituma kufanya biashara ndogondogo kwa mfano
lani ya kukidhi mahitaji ya familia, muhusik
a huyu anafaa kuigwa katika jamii ili kule
ta maendeleo ya jamii nzima.

Mwenye huruma; Katika riwaya hii tuna
ona pale mama ntiliye anapowaonea huruma watoto
wake akina Zitta na peter baada ya kufukuzwa
shuleni kwa sababu ya kukosa ada. Hivyo anaja
ribu kuanzisha biashara mbalimbali ambazo zitam
saidia kuingiza kipato ili aweze kuwalipia wana
e ada ya shule. pia katika jamii zetu wapo
akinamama wanaojitolea kwa moyo wa huruma
kuwalipia ada watoto wao, hata kama waume
zao wapo. hii ni ishara ya upendo ya wazazi
kwa watoto wao, pia inasaidia kuleta maendeleo
kwa jamii.

Mlezi wa familia- mlezi ni mtu ambaye
anachunga familia nzima kwa kuhakikisha kwa
mba wanafamilia wanapata mahitaji yao na pia
wanalelewa katika maadili mema. Mama ntiliye
ametumika kama mlezi wa familia, kwa saba
bu anahakikisha kwamba wanafamilia wame
pata chakula na mavazi na malazi. Pia kati
ka jamii zetu wapo wanawake ambao wana
chunga familia zao na kuhakikisha kwamb
a wanapata mahitaji muhimu. Pia kwa kutu

13. mia riwaya ya "JOKA LA MDIMU" msanii amemtumia mhusika Brown Kwacha katika kuonyesha hali halisi ya matukio ya kimaisha yanayotokea katika jamii kwa kupitia uhusika wake. Zifuatazo ni hoja ambazo msanii amezitumia kuonesha uhusika wa mhusika huyu;

Mtoa rushwa; katika riwaya hii tunaona jinsi Brown Kwacha akitoa rushwa kwa maofisa wa serikali wanaoshughulikia mambo ya ardhi ili apate kiwanja cha kujenga nyumba yake. pia katika jamii ya sasa, wapo viongozi wenye tabia kama hii ambao wanatumia uongozi wao kwa kuwanyanyasa wananchi.

Brown Kwacha anaonekana ni fisadi; ufisadi ni kitendo cha kujilimbikizia mali ya umma kwa ajili ya maslahi yako binafsi. Katika ~~ta~~ riwaya hii tunaona jinsi anavyotumia mali ya serikali kwa kujenga nyumba na kuendesha ukahaba na ufuska. Pia katika jamii yetu ya leo wapo watu hasa viongozi wenye tabia kama hii ya Brown Kwacha ambao wanatumia uongozi wao kwa kuhujumu mali ya nchi.

Malaya na mlevi; katika riwaya hii tunaona jinsi msanii anavyomtumia mhusika Brown Kwacha kuonyesha uhusika wake wa kuwa malaya na mlevi kufundisha jamii; pia katika jamii yetu ya sasa, pia wapo viongozi wanaotumia uongozi wao kwa kujiingiza kwenye ukahaba na ufuska wa kufanya ngono zisizo halali kwa sababu ya ulaji wa pesa ya jamii kwa ujumla.

| | |
|---|---|
| 13. | Kwa ujumla mwasanii wa riwaya zote |
| | mbili wameweza kuwatumia wahusika kama |
| | ipasavyo kwa kuwalenga wanajamii wanao |
| | jikita katika tabia kama zao hawa wahusi |
| | ka. Hatuna budi kushirikiana kwa wanaja |
| | mii wote ili tutekeleze baadhi ya tabia |
| | mbaya ambazo zinazuia kuleta maendeleo |
| | ya jamii zetu. |

Kielelezo 13.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na utangulizi sahihi kulingana na swali, hoja zenye ufafanuzi na alitoa hitimisho linaloendana na swali.

Watahiniwa wachache (21.4%) walipata alama 0 hadi 04, miongoni mwao asilimia 3.1 walipata alama 0, kwa sababu hawakujibu swali hili kwa usahihi. Watahiniwa hao badala ya kueleza kukubalika kwa wahusika waliopewa, walijikita katika kufafanua dhamira mbalimbali katika riwaya walizopewa. Hata hivyo, dhamira walizozifafanua hazihusiani kabisa na wahusika waliotakiwa kuwaelezea. Kielelezo 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea dhamira mbalimbali za riwaya badala ya kuelezea jinsi wahusika aliopewa walivyo kielelezo halisi cha maisha katika jamii.

**Kielelezo 13.2**

13 Kwa kutumia riwaya ya "TAKADINI" iliyoandikwa na BEN J. HANSON na riwaya ya WATOTO WA MAMA NTILIE iliyoandikwa EDWINI MBOGO Mwandishi amejadili kutokubalika kwa wahusika hao.

Kwa kuanza na riwaya ya TAKADINI mwandishi ameonyesha kutokubalika kama ifuatayo;

Ukombozi wa kiutamaduni; katika riwaya hii ya Takadini mwandishi ameeleza kuwa kuna baadhi ya watu wanawatendamiza na kuwanyonya watu ambao wana ulemavu wa ngozi. Mwandishi anamtumia mhusika Sekai kuwa ameonyesha ujasiri mtu bwa katika kumtorosha Takadini ambayo alikuwa na ulemavu wa ngozi (zeruzeru). Hivyo mwandishi ameonyesha kuwa hata kama mtu ni mlemavu anahaki ya kuishi kama watu wengine. Hii imeonyesha kutokubalika kumhusika huyu ambaye ni Sekai.

Ujasiri; katika riwaya hii mwandishi ameonekana kugusia suala la ujasiri kwani kuna baadhi ya watu wametumia mbinu ili kutomesha suala la kuwagandamiza walemavu kwani waliwaona hawana haki ya kuishi. Kwa mfano mhusika Sekai ambaye ni mama yake Takadini aliona si bora mwana o bufa bora aamue kumtorosha kwenda katika kijiji kingine ambacho ni kijiji cha Mzee Chivero na hatimaye alipotea kwa fulaha.

Nafasi ya mwanamke katika jamii; Hii ni sababu nyingine ambayo inaonyesha kutokubalika katika jamii. Ingawaye mwanamke anaonekana kama kiumbe duni, mtu asiyena msimamo, chombo cha starehe lakini pia mwanamke anaonekana kama mtu mwenye msimamo na mwanamapinduzi. Kwa kumtumia

mhusika Shingai alitukuwa mtu mwenye msimamo na aliyekuwa na mapenzi ya dati kwa Tatadini; Japokuwa wazazi wake hawakupenda Shingai kuolewa na tatadini lakini Shingai aliamua kutoroka nyumbani na hatimaye kuolewa na Tatadini.

Kwa kuendelea au kutumia riwaya ya ~~mama~~ Watoto wa Mama Ntilie mwandishi ameonyesha sinsi wahusika waliyokubalika katika jamii kama ifuatavyo;

Suala la Umaskini: katika riwaya hii tuna ona kuwa kuna Suala kubwa la Umaskini. Mwandishi anaonyesha kuwa suala la umaskini linakuwa misha baadhi ya mambo, kwa mfano katika wanafunzi kupata elimu inakuwa vigumu kwa sababu ya ukosefu wa pesa ambazo zitawasaidia wanafunzi kupata mahitaji kwa mfano ada na sale za shule ambapo mwalimu wao mkuu anawaambia "Kama huna sale na ada kesho usije". Hii inaonyesha kwamba baadhi ya familiya ni maskini.

Hatari za ulevi; Mwandishi anaeleza kuwa kuna baadhi ya wahusika ambao wameweka suala la ulevi kuwa ni kitu muhimu lakini mwandishi anaeleza kuwa Ulevi unaweza kusababisha familiya kutokuwa na usawa na pia kukosa malezi bora. Kwa mfano katika familia ya mzee lomolomo kulikuwa hakuna usawa kwani mzee huyu alikuwa anasihusisha katika ulevi tu na hatimaye kusababisha hata watoto wake kutoenda shule, kwani mke wake ndiye aliyekuwa akijishughulisha na kazi ya mama ntilie lakini pesa aliyopata inatosha mahitaji ya nyumbani. Hivyo mwandishi anaonyesha kukubalika kwa mhusika huyu.

13 Suala la elimu; katika riwaya hii ya Mam-
a ntilie mwandishi anaeleza kwamba suala la ele-
mu limetawa halitiliwi mkazo kwani wanafunzi w-
engi walikuwa hawaendi shule kwa sababu ya
sare na ada hatimaye mwalimu wao Mtuu Chu-
koya ataamua kuwafukuza na watoto hao wakaa
mua kujihusisha katika Ucambasi, wizi na madawa
ya kulevya, kwani kumfukuza mtoto shule eti sa
babu hana sare na ada sio kosa lake bali
ni kosa lawazazi.
Kwa hiyo katika hizi zote mbili tunaona kuwa
mwandishi amoonyesha kutukaliza kwa wahusika hao.
Huyo ni vizuri kwa siyo vizuri kuwakandamiza
watu ambao wana ~~Uta~~ ulemavu kwa mfano Pata-
dini.

Kielelezo 13.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika dhamira badala ya kuonesha kukubalika kwa wahusika katika riwaya.

### 2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali la 14 lilikuwa ni la *Fasihi Andishi* katika kipengele cha Tamthiliya na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli kuwa kazi ya kujenga jamii iliyo bora ni dhima ya mwandishi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15 na lilijibiwa na asilimia 79.2 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani.

Swali hili lilijibiwa vizuri sana kuliko maswali yote katika mtihani huu, kwani asilimia 93.8 walijibu swali hili kwa usahihi. Miongoni mwao asilimia 25.2 walipata alama $04^1/_2$ hadi $08^1/_2$, kwa sababu waliweza kuelezea baadhi tu ya hoja kwa usahihi. Aidha, asilimia 68.6 walipata alama 09 hadi 15, kwa kuwa waliweza kutoa hoja sahihi katika kuelezea kauli isemayo ‘kujenga jamii bora ni dhima ya mwandishi,’ aidha, walizifafanua hoja hizo kwa ufasaha zaidi. Kielelezo 14.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 14.1**

14. Mwandishi wa kazi za fasihi anatoa ujumbe mbal
mbali katika hadhira yake ambayo ni jamii nzima iliyo
mzunguka. Dhima yake kuu ni kuelimisha, kuonya na kukos
oa ili kujenga jamii bora. Kwa kutumia Tamthiliya ya
NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE iliyoandikwa na mwa
ndishi E. Senzaba na tamthiliya ya KILIO CHETU iliyoandikwa
na Medical Aid Foundation inathibitishwa kwa dhima kuu
ya mwandishi ni kujenga jamii bora. Tukianza na NGOSWE
PENZI KITOVU CHA UZEMBE ~~na~~ yafuatayo ni mambo ya
nayothibitisha madai hayo;
Ni lazima jamii kiepuke tabia ya ~~[illegible]~~ ulevi kwani
ni kikwazo cha maendeleo katika tamthiliya hii Mito
mingi anamkaribisha Ngowe pombe, wote wawili wana-

14. kunyuu kupitiliza na kusababisha kuchomwa na karatasi za sensa ya watu. Hiki ni kikwazo kwani Ngoswe hatoweza tena kupeleka takwimu serikalini. Hivyo mwandishi anaonya sana jamii juu la swala la ulevi kwani hunarudisha nyuma maendeleo ya jamii, hivyo ni lazima uepukwe.

Ndoa za mitala husababisha migogoro katika jamii hivyo mwandishi anakosoa ziachwe. Ndoa za mitala ni pale ambapo mwanaume anaoa wake wengi. katika tamthiya mzee Mitomingi alikuwa na wake wawili ilihali hali yake ni ya kimasikini. Inamuwia vigumu kukidhi mahitaji muhimu ya wake wote. kwaiyo mwandishi anajaribu aijenga jamii bora kwa kukebehi ndoa za mitala.

Imani potofu ziradumaza maendeleo ya jamii. Imani potofu ni imani zisizoza misingi ambapo watu wanajijengea kichwani mwao. katika tamthiliya tunaona jinsi Ngoswe anavyopata wakati mgumu kuhesabu watu kwani wengine wanaozani atawaloga. Jamii inahaswa kutupilia mbali imani potofu na kujikita katika maendeleo ya kijamii ili kuiboresha.

kwa upande mwingi tamthiya ya KILIO CHETU, mwandishi anaonekana kudhimia kutoa mafunzo ambayo yatajenga jamii bora. Yafuatayo ni uthibitisyo wa kauli hii

Ilimu ya kijinsia ni muhimu kwa watoto na vijana Mwandishi ameeleza jinsi jamii yetu sasa inavyoitaji kuweka vitu wazi ilikuokoa vijana. katika tamthiya mama suzi alishindwa kuweka mambo wazi kwa binti yake na matokeo yake akaishia kupata mimba na ukimwi Hivyo wazazi wanapaswa kuwaelimisha watoto wao juu ya Ilimu ya kijinsi ili kujenga jamii iliyo bora.

Maadili ni lazima yaingatiwe ili kujenga jamii iliyo bora. Mwandishi anasisitiza sana juu ya maelezo la tabia ... tabia zote mbaya katika tamthiliya

14. mwandishi anamtumia Joti kuonyesha jinsi jamii ilivyooza
Joti anajikita katika kuangalia sinema za ngono na mang
bo ya mapenzi wakati umri wake ni mdogo. Mwandishi
anaeleza wazi kabisa juu ya hatari ya mmomonyoko wa
maadili hivyo anaiboresha jamii kwa kukemea vikali tabia
mbaya.

Mwisho, mwandishi anachasa kwamba UKIMWI ni
hatari katika jamii yetu. Mwandishi amoonesha kwamba
Ukimwi hauchagui dini, umri wala jinsia. Joti na Suzi wa
lipata ukimwi japo umri wao ulikuwa mdogo, Joti alia
fa kwa UKIMWI. Mwandishi anaonesha ni jinsi gani Uki
mwi unaweza kupoteza nguvu kazi za jamii hivyo ni
lazima tuwepuke. Mwandishi anaiboresha jamii.

Hivyo basi, ni dhamira ya kila mwandishi kuadabisha
na kueleza mambo muhimu kwa jamii ilikujenga jamii
iliyobora. Mwandishi yoyote yule atakaze sana juu ya
mambo ambayo jamii hawapaswi kufanya na juu ya
mambo ambayo yanatakiwa kufuatwa ili kujenga jamii
iliyobora.

Kielelezo 14.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua kuwa kazi ya kujenga jamii bora ni dhima ya mwandishi.

Watahiniwa wachache sana (6.2%) ndio waliojibu swali hili vibaya na kupata alama 0 hadi 04, miongoni mwao asilimia 1.5 walipata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kufafanua jinsi mwandishi anavyojenga jamii bora kwa kutumia dhima zilizopo katika tamthiliya yake. Kielelezo 14.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo 14.2**

14 Kwa kuanza na tamthiliya ya Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe kilichoandikwa na Edwin Semzaba (ESC) ~~tunaona kuwa mwandishi amemwo~~

14 Zifuatazo ni kauli ambazo zinathibitisha jinsi mwandishi anavyojenga jamii

Kumchora Ngoswe kama ni mtu ambaye hafai katika jamii – Mwandishi amemchora ngoswe kama ni kijana ambae hafai kuigwa katika jamii kutokana na matendo yake yaliyoridhisha. Hii ni njia ambayo ametumia mwandishi katika kuelimisha jamii.

Amemchora mitomingi kama mzee ambae hana elimu Hii ni njia mojawapo ambayo ameitumia mwandishi kumuonesha wanajamii kuwa haifai kuchukua hatua kama vile ambavyo alifanya mitomingi. Hii ni njia nyingine ambayo alitumia mwandishi.

Amemchora Mazoea kama msichana ambae hana maamuzi mazuri – Mwandishi amethibitisha hili kwa kuonyesha hali kwa mazoea ametoroshwa kwa kushawishika na Ngoswe ile ni picha tosha ambayo itamfanya mwanajamii yoyote kuzingatia hayo.

Kwa kumalizia na tamthiliya ya Ngoswe Penzi kitovu cha Uzembe tunaangalia tamthilia ya kilio chetu ambayo imeandikwa na Medical Aid Foundation (TPH)

Mary kutomsikiliza mzazi wake – Hili ni jambo ambalo mwandishi ameliweka wazi kuwa baadhi ya watoto hawawasikilizi wazazi wao na kufanya yale wanayoyaamulia wao binafsi

Kielelezo 14.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeelezea wahusika badala ya kuelezea dhima ya msanii katika kujenga jamii bora.

### 2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Kazi za Kifasihi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utungaji wa Kazi za Kifasihi* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuunda mawazo. Swali liliwataka watahiniwa watunge tamthiliya fupi yenye maneno yasiyopungua 300 kuhusu Umuhimu wa Elimu kwa Vijana wa Tanzania. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15 na lilikuwa ni la lazima.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wengi (98.1%). Katika swali hili mtahiniwa alipaswa kutunga tamthiliya kwa kuzingatia: *kichwa cha tamthiliya, tendo linalotendeka, mahali tendo linapofanyikia, watendaji, watazamaji, matumizi ya lugha, matumizi ya alama za uandishi na vituo pamoja na idadi ya maneno.*

Zaidi ya nusu ya watahiniwa sawa na asilimia 69.7 walijibu swali hili vibaya na walipata alama 0 hadi 04 miongoni mwao asilimia 41.7 walipata alama 0. Watahiniwa hao waliandika tamthiliya ambazo hazikuzingatia taratibu za uandishi wa tamthiliya. Aidha, watahiniwa wengine waliandika hadithi zenye maneno zaidi ya 200 yaliyo kwenye mtiririko wa aya moja tu, na wengine waliandika mashairi badala ya tamthiliya. Kielelezo 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kabisa kutunga tamthiliya.

**Kielelezo 15.1**

15. Kutunga tamthilia ya fupi kuhusu umuhimu wa elimu kwa vijana wa Tanzania ya leo

UMUHIMU WA ELIMU

1. Elimu kwa vijana, ni muhimu
Yafaa kuifanyia, kweli
Itainua uchumi Tanzania, kwa kujitolea
tuboreshe elimu Tanzania, vijana kuboresha

2. Uchumi utakua, vijana wakijipatia
Umasikini utapungua, vijana kwenye ajira
Shida zao zitapotea, mshara kujipatia
tuboreshe elimu Tanzania, vijana kuboresha

3. Elimu chanzo cha maendeleo, Tanzania kuinuka
Kwanza kufuta mambo leo, Tanzania kusifika
Janani naomba kutuamkazo, uchumi kuinuka
tuboreshe elimu Tanzania. Vijana kuboresha

4. Kwa kasi vijana kuinua uchumi, mabadiliko kutokea
kutia kipato hapa nchini, vijana kuangalia
Vijana kufuta umasikini, maendeleo kidyaleta
tuboreshe elimu Tanzania, vijana kuboresha

5. Vijana ni wachapa kazi, bila ya mapema kudhaa
Tena hawana simanzi, migogoro kusikika
Wakweli pia wawazi, kipato kukifikisha
tuboreshe elimu Tanzania, vijana kuboresha

Kielelezo 15.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetunga shairi badala ya tamthiliya.

Asilimia 30.3 tu ya watahiniwa ndio waliozingatia taratibu za uandishi wa tamthiliya. Miongoni mwao asilimia 15.1 walipata alama $04^1/_2$ hadi $08^1/_2$, kwa kuwa walizingatia taratibu chache za uandishi. Asilimia 15.2 walizingatia kwa kiasi kikubwa taratibu za uandishi wa tamthiliya hivyo waliweza kupata alama 09 hadi 15. Kielelezo 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali vizuri.

**Kielelezo 15.1**

15. TAMTHILIA KUHUSU UMUHIMU WA ELIMU KWA VIJANA WA TANZANIA YA LEO.

Wahusika

- Kardi - kaka wa Happy
- Happy dada wa Kardi
- Kapela ndugu wa Kardi na Happy.
- Mzee Martin

SURA YA KWANZA.

Ilikuwa asubuhi na mapema, ndipo wahusika walipokuwa wameonekana wameketi nje ya nyumba ya mzee Martin wakiwa wanajishughulisha na shughuli mbalimbali.

Kardi: Nilimsikia baba jana akiwa anazungumza juu ya masuala ya vijana wa leo kuwa wanaonekana kuwa Tanzania ya leo. (Huku akiendelea kufua nguo).

Happy: Ndio kaka maana yeye alisema hivyo akijiona kuwa ameanza kuzeeka (naye akiwa anaosha vyombo).

Kardi: Hata hivyo sisi vijana inatupasa kutambua wajibu wetu katika taifa letu la Tanzania ili tuhakikishe tunalijenga kwa umahiri (mara baba akatoka ndani).

Mzee Martin: Mhuh! Hamjambo wanangu (wote waliitikia wakiendelea na shughuli zao) naona mnafanya shughuli za usafi ni vyema mkajitahidi kumaliza mapema ili muwahi kanisani maana kuna semina ya vijana leo.

Kardi: Aah! Ndio baba tunakushukuru mimi na dada yangu tutajitahidi kumaliza mapema kazi zetu

Happy: lakini baba, tunakuomba utuachie hata hela ya maji pindi tutakapokuwa huko maana hatujui semina itaisha saa ngapi.

Mzee Martin: Sawa mwanangu (alijibu huku akiingia ndani).

Happy : Kaka tunashukuru kuwa baba ametukumbusha kuhusu ile semina ya vijana maana leo tutajifunza juu ya umuhimu wa vijana katika taifa letu la Tanzania. (akizunguma huku akiendelea kuosha vyombo).

Karoli : Ndio mdogo wangu hivyo fanya haraka ili tuweze kuwahi (baba alitoka na kuwapatia hela ya chai na ya chakula pindi watakapokuwa kwenye semina).

lakini tusisahau kumpitia ndugu yetu kapela.

SURA YA PILI

Padri : Karibuni vijana wote katika semina yetu ya leo ya kujifunza juu ya umuhimu wa ~~vijana~~ ~~ka~~ elimu kwenu nyinyi vijana wa leo. (Padri aliendelea kuwakaribisha vijana hao huku akijiandaa kuanzisha elimu hiyo).

Padri : Kwanza ni lazima tujue nini maana ya vijana, Hivyo mmoja wetu atusaidie.


Happy : Mimi ninavyoelewa vijana maana yake ni watu waliofikia umri wa miaka kumi na nane hadi 30 ambao hufanya mambo kwa kujielewa
(alijibu akiwa amesimama na kupigiwa makofi)

Padri : Vizuri, hivyo wote tumepata kujua maana ya kijana. Vijana wa Tanzania ya leo wamekuwa wakipotea na kufanya mambo ya ajabu ambayo hayastahili mbele ya Mungu na mbele ya jamii (alisimama kidogo akiwa anaandika ubaoni).

Padri : Hivyo ni lazima mpate elimu ili muweze kujitambua na kufanya mambo yaliyosahihi. Hivyo upatao ni umuhimu wa elimu kwa vijana wa Tanzania ya leo.

Padri : Vijana mkielimishwa mtaweza kujitambua na hivyo kuepuka masuala yote ambayo hayafai katika jamii (alisimama kidogo akimuluhusu swali).

Karoli : Tutajuaje kuwa tumejitambua.


SURA YA TATU.

Padri: Hivyo ni rahisi kijana yeyote anayejitambua kuweri kufanya mambo ambayo hayapendezi kama vile utumiaji wa bangi.

Sista: Hata hivyo mkielimishwa ningi vijana mtaweza kuepukana na makundi maovu yote na kushikamana kwa pamoja.

mfano:- vijana wengi wamekuwa wakifuata milegezo, wakijihusisha na utumiaji wa madawa ya kulevya kwa maana walikuwa hawana elimu juu ya mambo ya hivyo ndiyo.

Sista: Pia vijana mkielimishwa maovu katika jamii yatapungua na hivyo tutajenga jamii iliyobora.

Padri: Hata hivyo vijana mnaweza mkakombolewa katika majanga yote ya maradhi kama vile UKIMWI endapo mtapewa elimu juu ya ugonjwa huo.

Padri: Vijana pia mnaweza kuleta maendeleo makubwa katika nchi yenu pindi mtakapoelimishwa juu ya matumizi ya rasilimali zilizopo kupitia elimu.

Hizo zote tulizowaeleza ni umuhimu wa elimu kwenu nyinyi vijana wa Tanzania ya leo.

Happy: Asante sana ndugu padri kwani mmeweza kutueleza mambo mbalimbali ambayo nilikuwa siyafahamu na hii kumbe ndio umuhimu wa elimu kwetu sisi vijana wa Tanzania ya leo.

Kardi na kapela: Hata sisi pia tumeweza kujua mambo mbalimbali ambayo tulikuwa hatuyafahamu. Hivyo tunashukuru sana.

Vijana hao waliweza kujifunza juu ya umuhimu wa elimu kwa vijana wa Tanzania ya leo na hivyo walikuwa tayari kuwaelimisha wenzao. MWISHO.

Kielelezo 15.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyezingatia taratibu za uandishi wa tamthiliya.

## 3.0 HITIMISHO

Katika somo la Kiswahili, mada zilizotahiniwa zilikuwa ni *Ufahamu na Ufupisho, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali, Aina za Maneno, Uundaji wa Maneno, Uandishi, Maendeleo ya Kiswahili, Fasihi Simulizi, Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* na *Kutunga Kazi za Fasihi.* Mada nane (8) kati ya kumi na moja (11) zilizotahiniwa zilijibiwa vizuri, mada mbili zilijibiwa kwa kiwango cha wastani na moja haikujibiwa vizuri kwani kiwango chake kilikuwa ni hafifu.

Mada zilizofanyika vizuri katika somo la **Kiswahili** *ni Uhakiki wa Fasihi Andishi* katika Tamthiliya na Riwaya , *Uandishi , Fasihi Simulizi, Aina za Maneno, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na *Uundaji wa Maneno.*

Mada za *Maendeleo ya Kiswahili* na *Ufahamu na Ufupisho* ambazo mwaka 2013 zilifanyika vizuri, kwa mwaka 2014 zimefanyika kwa kiwango cha wastani. Mada za *Uundaji wa Maneno* na *Utungaji wa Kazi za Kifasihi* ambazo zilikuwa za kiwango hafifu kwa mwaka 2013, kwa mwaka 2014 zimefanyika kwa kiwango cha wastani. Aidha mada ya *Uhakiki wa Fasihi Andishi* katika Ushairi ndiyo mada pekee ambayo haikujibiwa vizuri kwa mwaka 2014 pamoja na kwamba mwaka 2013 mada hii ilikuwa miongoni mwa mada zilizojibiwa vizuri kwa wastani wa ufaulu wa 60.2% lakini wastani wa ufaulu kwa mwaka 2014 ni 24.1% ambao ni hafifu.

Mada ya *Uhakiki Fasihi Andishi katika Ushairi* haikujibiwa vizuri kwa sababu, watahiniwa hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusiana na mada hiyo. Watahiniwa wengi wamekuwa na tatizo la kutokuchambua kwa kina mada ya *Uhakiki wa Ushairi* kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui. Aidha, uchambuzi wa fani unahitaji uelewa wa kina wa kazi ya fasihi husika kwa vile unahusisha vipengele vingi kama vile wahusika, lugha na mandhari ambavyo vinahitaji uelewa wa kutosha. Hivyo, watahiniwa hao walikosa ujuzi na maarifa kuhusu mbinu za kiuchambuzi hasa katika kuzingatia kipengele cha lugha ambacho ni muhimu mno katika kufikisha ujumbe wa kazi za Fasihi Andishi.

Ingawa somo la Kiswahili limefanyika vizuri na ufaulu wa watahiniwa ni wa kiwango kizuri mkazo wa ufundishaji na ujifunzaji wa mada za *Maendeleo ya Kiswahili na Utungaji wa Kazi za Fasihi Andishi* uongezwe ili kuwe na ufaulu mzuri katika mada hizi ambazo ufaulu wake kwa mwaka huu umekuwa ni wastani. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya *Uhakiki wa Kazi*

*za Fasihi Andishi* (Ushairi) ili kuongeza zaidi kiwango cha ufaulu katika mada hii ambayo ufaulu wake umeshuka sana.

Taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu wa somo hili kwa kuwa itakuwa changamoto kwa walimu katika ufundishaji wa mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Uundaji wa Maneno*, *Maendeleo ya Kiswahili*, *Uhakiki wa Fasihi Andishi* kipengele cha ushairi na *Utunzi wa Kazi za Fasihi*.

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo hili inapendekezwa kuwa;

(a) Walimu wazingatie muhtasari wa somo wanapofundisha mada mbalimbali. Aidha, waweke mkazo katika ufundishaji wa mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Uundaji wa Maneno*, *Maendeleo ya Kiswahili*, *Uhakiki wa Fasihi Andishi kipengele cha ushairi* na *Utunzi wa Kazi za Fasihi*.

(b) Wanafunzi wahamasishwe kujishughulisha zaidi katika stadi za utunzi wa kazi za kifasihi.

(c) Ufundishaji wa kipengele cha fani katika kazi za Fasihi Andishi utiliwe mkazo.

(d) Walimu wawahimize wanafunzi kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu.

(e) Wanafunzi wahamasishwe kujihusisha katika mada ya *Uhakiki wa Fasihi Andishi kipengele cha Ushairi* na hasa kusoma na kuchambua mashairi. Aidha, mazoezi ya utunzi na uhakiki wa ushairi yatiliwe mkazo zaidi.

(f) Walimu watoe mazoezi/majaribio mengi yanayohusu mada mbalimbali ili kuwapima wanafunzi na kuwapa uwezo mkubwa wa kufahamu mada mbalimbali na matakwa ya aina mbalimbali za maswali.

**Kiambatisho**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

## SOMO LA KISWAHILI

| Na | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya watahiniwa waliopata wastani wa asilimia 30 au zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uhakiki wa Fasihi Andishi Tamthiliya | 14 | 93.8 | Vizuri |
| 2 | Uandishi | 8 na 9 | 86.7 | Vizuri |
| 3 | Uhakiki wa Fasihi Andishi Riwaya | 13 | 78.6 | Vizuri |
| 4 | Fasihi Simulizi | 11 | 66.3 | Vizuri |
| 5 | Aina za Maneno | 4 na 7 | 65.0 | Vizuri |
| 6 | Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali | 3 | 64.5 | Vizuri |
| 7 | Uundaji wa Maneno | 5 na 6 | 54.0 | Vizuri |
| 8 | Ufahamu na Ufupisho | 1 na 2 | 53.9 | Vizuri |
| 9 | Maendeleo ya Kiswahili | 10 | 33.9 | Wastani |
| 10 | Kutunga Kazi za Fasihi | 15 | 30.3 | Wastani |
| 11 | Uhakiki wa Fasihi Andishi Ushairi | 12 | 24.1 | Hafifu |